JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbclindi@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

**LINDI – JULAI, 2022**

# WADAU MKOA WA LINDI WASISITIZA KUFANYIKA KWA MAPITIO YA SHERIA NDOGO ZA TOZO YA HUDUMA INAYOZIDI KIWANGO CHA SHERIA MAMA YA MADINI ILI KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Aprili hadi Juni, 2022, msisitizo mkubwa ukiwa katika kuzuia rushwa ambapo elimu ya kuhamasisha wananchi ili washiriki kikamilifu kuzuia rushwa ilipewa msukumo mkubwa kwa kuwa rushwa inarudisha nyuma maendeleo na matumaini ya jamii.

Aidha kupitia kazi za Uzuiaji Rushwa za kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa mapato yanayotokana na ushuru wa madini ujenzi, wadau walioshirikishwa walizitaka halmashauri za mkoa wa Lindi, kufanyike mapitio ya sheria ndogo ya ada na ushuru wa madini ya ujenzi inayozidi kiwango cha sheria mama ya madini, ili kuzuia mazingira ya mianya au vitendo vya rushwa vinavyotokea kutokana uwepo wa mapungufu haya.

## UELIMISHAJI UMMA:

Ukilinganisha kazi za uelimishaji zilizofanyika katika robo hii mwaka jana, kuna ongezeko la asilimia 40 la kazi za uelimishaji kwa robo ya mwaka huu. **Kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:**

| Na. | KAZI | UFAFANUZI |
|---|---|---|
| 1 | Elimu ya kubadili mtizamo wa makundi ya wananchi ili watambue wajibu wao wa kushiriki kivitendo kuzuia vitendo vya rushwa kabla ya kutokea | Elimu hii ilitolewa kwa kulenga rika la vijana kupitia klabu za wapinga rushwa na kuelimisha wanachama wa SKAUTI kupitia mkakati wa ushirikiano kati ya TAKUKURU na SKAUTI |
| 2 | Mpango maalum wa TAKUKURU INAYOTEMBEA, kwa kuwafuata watu walipo na kusikiliza kero za wananchi. | Elimu ya rushwa ilitolewa kwa kundi la waendesha bodaboda katika halmashauri ya manispaa ya Lindi walipotembelewa baada ya kusikilizwa kero zao.<br>• Mpango huu maalumu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA ulifanikiwa kufikia vijiwe/vikundi 20 vya bodaboda ambapo waendesha pikipiki 300 walifikiwa na kusikilizwa kero zao.<br>• Baadhi ya kero zao zilipatiwa ufumbuzi wa papo kwa papo na nyingine ambazo hazikupata majibu zilichukuliwa ili kufikishwa mamlaka zinazohusika kufanyiwa kazi na kutolewa majibu.<br>• Elimu ya rushwa iliyotolewa baada ya kusikiliza kero zao ilisisitiza umuhimu wao katika kuzuia rushwa badala ya kuwa watazamaji kwa manufaa ya kazi yao pamoja na maendeleo na ustawi jamii kwa ujumla. |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Tunaendelea kuwahimiza walioelimishwa kuwa mabalozi wetu kwa kupeleka elimu waliyoipata kwa wananchi wengine na kuwa mfano wa mabadiliko kwa vitendo katika kuzuia rushwa badala ya kuamini kuwa jukumu hili ni la serikali pekee. |
| 3 | Kutembelea na kuziimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo. | Klabu za Wapinga Rushwa zimetembelewa mara 104<br>- Kumekuwa na mwamko mkubwa wa vijana katika kupinga rushwa baada ya kufundishwa kuwa waadilifu, wawajibikaji na wazalendo zaidi katika jamii na taifa kwa ujumla. |
| 4 | Semina ya kuhamasisha nafasi ya walimu walezi wa klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi na sekondari pamoja na walimu walezi wa Skauti | Kupitia Semina hii, mikakati ya kuziimarisha Klabu za Wapinga Rushwa na utekelezaji wa mpango wa TAKUSKA iliwekwa |
| 5 | Uandaaji na urushaji wa vipindi vya redio 9 | Elimu ya rushwa iliyotolewa imelenga kuwakumbusha na kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu na wajibu wa wananchi wa mkoa wa Lindi katika kushiriki kuzuia rushwa. |
| 6 | Maonesho | Wananchi walihamasishwa kushiriki katika kuzuia vitendo vya rushwa . |
| 7 | Semina 14 zimetolewa kwa watumishi wa umma na sekta binafsi. | Elimu ya rushwa iliyotolewa kwa kundi hili ni kuhusu wajibu walio nao katika kuzuia vitendo vya rushwa |

Aidha, elimu ya rushwa ilitolewa kupitia mikutano ya hadhara 6 na uandishi wa makala 8 za visa vya rushwa.

**Pili,** katika eneo la **UZUIAJI RUSHWA,** TAKUKURU Mkoa wa Lindi imefuatilia utekelezaji wa miradi 15 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.87 (3,869,104,909.84) katika sekta za Maji, Afya na Elimu. Hii inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19.

- Miradi 1 (sawa na asilimia 7), ulikuwa na mapungufu madogo ambayo ni upokeaji wa vifaa na utoaji kufanywa na mtu mmoja hivyo kutokuwa na ushirikishaji wa kamati za mapokezi hali inayopelekea kutokuwa na uhakiki wa kamati pamoja na taarifa ya mapokezi na utoaji.
- Wasimamizi wakuu wa mradi unaotekelezwa kwa nguvu kazi ngazi ya halmashauri kuishi mjini ambapo ni mbali na eneo la mradi unapotekelezwa hivyo kukosekana kwa maelekezo kwa mafundi kwa wakati.
- Mapungufu husika yalirekebishwa kwa kutoa elimu na kusimamia marekebisho kwa kushirikiana na wadau.

TAKUKURU Lindi ilifanya **uchambuzi wa mfumo** ili kubaini iwapo kuna mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuiziba katika maeneo ya utendaji au utoaji wa huduma yaliyoonekana au kulalamikiwa kuwa na viashiria vya rushwa kama ifuatavyo:

- Tumefanya **chambuzi mbili** za mifumo katika sekta za mapato na manunuzi.
- Tumebaini kwamba, pamoja na mambo mengine, kutokana na sheria ndogo ya ada na ushuru wa madini ya ujenzi za halmashauri kuzidi kiwango cha sheria mama ya madini, imekuwa ni chanzo cha kusababisa mazingira ya mianya au vitendo vya rushwa (mfano, sheria ndogo ya mwaka 2019 ya halmashauri ya Manispaa ya Lindi).
- Aidha, halmashauri zinapoteza fedha za miradi inayotekelezwa kwa nguvu kazi ngazi ya halmashauri kutokana na Ufujaji wa Mafuta katika Mradi wa Ujenzi na kutojazwa kwa madaftari ya kuratibu Safari (LOGBOOK) kuthibitisha uhalali wa matumizi ya mafuta ya mradi (mfano, ujenzi wa shule).

- **Warsha tatu** za kujadili matokeo ya uchambuzi wa mifumo kwa kushirikisha wadau zilifanyika katika sekta za Mapato, Elimu, ujenzi na uchukuzi ambapo maazimio ya namna ya kuziba mianya ya rushwa yalifikiwa na muda wa utekelezaji kuwekwa. Vilevile, taarifa moja ya utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa siku za nyuma katika sekta za ardhi na afya ilipokelewa.

**Tatu,** Licha ya kuhamasisha sana kuhusu **KUZUIA RUSHWA**, kuna jumla ya **malalamiko 42** tuliyopokea ambapo taarifa za rushwa zilikuwa **19** na zisizo za rushwa ni **23**. Taarifa hizi zilizopokelewa ni nusu ukilinganisha na taarifa zilizopokelewa katika robo kama hii mwaka 2021 hali ambayo inaashiria kuwepo kwa mafanikio katika mikakati ya kuzuia rushwa.

- Taarifa 19 zilizohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo: Serikali za mitaa (6); Mahakama (4), Ushirika (3), Afya (2), Elimu, Fedha, Maji, Biashara (kila moja 1). Taarifa hizo, zimeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwa njia za uelimishaji, uzuiaji pamoja na uchunguzi.
- Katika kipindi hiki, Majalada 3 ya uchunguzi yamekamilika na mashauri **6** mapya yamefunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani kufikia **16**.
- Kwa taarifa **23** zisizohusu rushwa, 3 zilihamishiwa idara zingine na wahusika wa taarifa 20 zilizosalia walishauriwa mahali sahihi pa kuziwasilisha kwa msaada na hivyo taarifa hizo zikafungwa.
- Taarifa 14 zisizohusu rushwa zilihusu Serikali za Mitaa.

**Nne, MIKAKATI YA JULAI – SEPTEMBA, 2022**

TAKUKURU Mkoa wa Lindi, imejipanga katika robo ya kwanza ya mwaka inayoanzia Julai - Septemba, 2022 itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuendelea kudhibiti vitendo vya rushwa katika ununuzi wa umma, ukusanyaji wa mapato ya Serikali, huduma muhimu, ufuatiliaji wa rasilimali za umma katika miradi ya maendeleo na kukuza ushirikiano na wadau kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Lindi itaendelea kuchunguza na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma na kwa kushirikiana na ofisi ya Taifa ya Mashtaka itawafikisha mahakamani watuhumiwa wa vitendo vya rushwa.

**SENSA KWA MAENDELEO YA TAIFA JIANDAE KUHESABIWA**

**Imetolewa na:**



Justine K. Maingu

**Kaimu Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi**

0754896221/0738 150 118

(26)


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Mtaa wa Sheikhbad,
S.L.P. 1004,
65101LINDI,
Barua Pepe: rbclindi@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**
www.pccb.go.tz


**LINDI – APRILI, 2022**

# TAKUKURU LINDI YAENDESHA MAFUNZO KWA WATENDAJI NA KUFANYA UFUATILIAJI WA MIRADI YENYE THAMANI YA SHILINGI 3,744,489,057/=

**Ndugu wanahabari,**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi inajumuisha ofisi za TAKUKURU Lindi Mkoani pamoja na zilizoko katika wilaya za Kilwa, Nachingwea, Liwale na Ruangwa. Majukumu yetu yalitekelezwa kupitia madawati mbalimbali ikiwemo Dawati la Uchunguzi, Huduma za Sheria na Mashtaka, Uzuiaji Rushwa pamoja na Elimu kwa Umma.

**Ndugu wanahabari,**

**UCHUNGUZI NA MASHTAKA:**

Kwa kipindi cha Januari, 2022 hadi Machi, 2022 TAKUKURU Mkoa wa Lindi imepokea jumla ya taarifa za malalamiko **72** Kati ya taarifa hizo, **48** zilihusu tuhuma za Rushwa na taarifa **24** hazikuhusu Rushwa. Kati ya taarifa hizo **48** zilizohusu Rushwa majalada **34** yanaendelea na uchunguzi, majada **4** uchunguzi umekamilika na majalada **10** yamefungwa.

Taarifa **24** zisizohusu rushwa, taarifa **9** zimehamishiwa idara nyingine kwa hatua zaidi na taarifa **15** watoa taarifa wameelimishwa na kushauriwa.

**Ndugu wanahabari,**
Kwa upande wa mashtaka katika kipindi hiki, TAKUKURU (M) Lindi ilifanikiwa kufungua mashauri **2** katika Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa na Kilwa na kufanya jumla ya mashauri kumi **(14)** yanayoendelea kusikilizwa mahakamani.

**Ndugu wanahabari,**
**UZUIAJI RUSHWA:**
Jukumu lingine la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni kufuatilia matumizi ya rasilimali za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ufuatiliaji huu unalenga kubainisha yafuatayo: Mianya ya rushwa; Ucheleweshaji wa utekelezaji; Uvujaji; na Ushirikishwaji wa wananchi/wadau.

Katika kipindi hiki TAKUKURU Mkoa wa Lindi ilifuatilia matumizi ya fedha za Miradi kumi na nane (18) ya Maendeleo yenye jumla ya thamani ya Shilingi **3,744,489,057/=.** Mradi miwili (2) iliyofanyiwa ufuatiliaji yenye thamani ya shilingi **928,340,557/=** ilikuwa na kasoro ya kucheleweshaji kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hii. Elimu imetolewa kwa wadau wa miradi hii ili kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kusisitiza uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma ili kupata miradi bora yenye kukidhi thamani ya fedha (Value for money) kwa wakati. Jumla ya miradi kumi na sita (16) yenye thamani ya shilingi **2,774,489,057**/= iliyofanyiwa ufuatiliaji haikuwa na kasoro.

**Uimarishaji wa mifumo** hufanyika kwa kufanya uchambuzi wa mifumo, kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufuatilia utekelezaji wa mikakati. Uimarishaji huo ulihusisha uchambuzi wa mfumo wa huduma za matengenezo ya magari chini ya TEMESA.

**Malengo ya uchambuzi huu ni:** Kuainisha mafanikio katika utoaji wa huduma za matengenezo ya magari; Kuanisha changamoto katika utoaji wa huduma za matengenezo ya magari; Kuainisha fursa zinazoweza kusaidia uboreshaji wa utoaji wa huduma za utengenezaji wa magari na; Kuainisha vihatarishi vya rushwa katika utoaji wa huduma za matengenezo ya magari.

**Matokeo ya Uchambuzi:**

Kupitia uchambuzi huu, ipo mianya ya rushwa iliyobainishwa ambayo kupitia warsha inayotegemewa kufanyika hivi karibuni, tutakaa na wadau husika ili kujadili matokeo ya uchambuzi wetu na kuwekeana maazimio ya namna bora ya kuondokana na mianya hiyo ya rushwa na baadaye kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa.

**Ndugu wanahabari,**
**UELIMISHAJI UMMA:**

TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendelea kutekeleza malengo yake ya Dawati la Elimu kwa Umma kwa kuwaelimisha wananchi wa makundi mbalimbali na wadau wengine kuhusu rushwa na madhara yake kwa mtu mmoja mmoja, jamii, taasisi na taifa kwa ujumla.

TAKUKURU Mkoa wa Lindi imeendesha semina 19, imefanya mikutano ya hadhara 38. Pia TAKUKURU (M) Lindi imefanya uimarishaji wa klabu za wanafunzi za wapinga rushwa 26, vipindi vya redio 2 na Utoaji wa makala au uandishi wa habari 4.

**Ndugu wanahabari,**
**TAKUKURU INAYOTEMBEA**:

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 katika kufahamu na kuzifanyia kazi kero za wananchi TAKUKURU imeendelea na mpango wa TAKUKURU INAYOTEMBEA. Kwa kutekeleza mpango huu, TAKUKURU Mkoa wa Lindi huambatana na baadhi ya Wakuu wa Idara za Halmashauri na mamlaka nyingine ili kuweza kutatua kero za wananchi papo kwa papo na zile

ambazo zinakuwa hazina majibu ya mara moja, huchukuliwa na kufanyiwa kazi na majibu kutolewa.

Katika kipindi hiki, wananchi wengi wamejitokeza na kulalamikia huduma mbovu za Afya katika Zahanati na vituo vya afya, uhaba wa dawa katika vituo vya afya, ubovu wa barabara maeneo ya vijijini na kuondolewa kwa wachimba madini wadogo dogo katika eneo ambalo walianza kuchimba kabla ya mwekezaji anayedai eneo hilo kuwa lake kujitokeza katika kijiji cha Chingumbwa, kutokulipwa malipo ya mauzo ya korosho zao kwa maelezo ya korosho kuwa chafu licha ya korosho zao walizopeleka chamani kuwa safi na upendeleo/mianya ya rushwa katika kuungiwa umeme wa REA 2.

TAKUKURU mkoa wa Lindi ikishirikiana na idara za Halmashauri, Tanesco, TARURA na mamlaka zingine inaendelea kushughulikia malalamiko mbalimbali yanayoibuliwa katika kipindi hiki kufuatia mpango huu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA.

Aidha hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwaagiza viongozi wa ngazi ya vijiji na kata kubandika kwenye mbao za matangazo miradi inayotekelezwa, kusomwa kwa mapato na matumizi ya miradi inayosimamiwa katika maeneo ya vijiji na kata.

**USHIRIKIANO NA SKAUTI (TAKUSKA)**

Katika kipindi hiki, TAKUKURU mkoa wa Lindi imeendelea na utekelezaji wa mpango wa TAKUSKA kwa kuendesha Mafunzo kwa maafisa elimu wa halmashauri za wilaya, maafisa elimu kata, viongozi wa makundi wa skauti, walimu walezi wa klabu za wapinga rushwa, wakuu wa shule na walimu wakuu katika halmashauri ya manispaa ya Lindi, Mtama, Nachingwea na Ruangwa. Aidha kanzi data kwa kila wilaya na ngazi ya mkoa inaendelea kuandaliwa kupatikana idadi ya vijana wa Skauti ngazi ya wilaya na mkoa.

**Ndugu wanahabari,**

Katika kipindi hiki tumeendelea na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Jumla ya miradi saba (7) yenye thamani ya shilingi 8,620,000,000/= ambayo iko hatua ya mwisho ya utekelezaji imeendelea kufanyiwa ufuatiliaji.

**Ndugu wanahabari,**

**MAADHIMISHO:**

TAKUKURU Mkoa wa Lindi ilishiriki katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini pamoja na wadau wengine wa Haki-Jinai kwa kushiriki katika uelimishaji umma kupitia redio Mashujaa pamoja na uelimishaji katika taasisi juu ya **safari ya maboresho kuelekea mahakama mtandao na wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa**. Taasisi zilizotembelewa na TAKUKURU Lindi pamoja na wadau wengine wa Haki-Jinai, katika kipindi hiki wakati wa maadhimisho ya wiki ya sheria ni Magereza, Lindi sekondari, chuo cha mafunzo ya utabibu Lindi (COTC) na chuo cha mafunzo na ufundi stadi Lindi (VETA).

**Ndugu wanahabari,**

**MIKAKATI YA APRILI – JUNI, 2022**

Katika robo ya nne (4) ya mwaka wa fedha 2021/2022 inayoanza Aprili, 2022 hadi Juni, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Lindi imejipanga katika kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa fedha za Miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri zote ndani ya mkoa wa Lindi. Pia Mkoa umejipanga kukamilisha chunguzi zinazotokana na taarifa mbalimbali pamoja na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na nyinginezo.

Kwa upande wa uelimishaji umma, sambamba na kuendelea kuelimisha umma kuhusu madhara yatokanayo na vitendo vya rushwa, pia katika kuhakikisha kuwa tunaendelea kuwafikia vijana wengi zaidi, TAKUKURU mkoa wa Lindi kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya mkoa, itaendelea na Utekelezaji wa Mpango Kazi wa TAKUSKA kwa lengo la

kuwezesha ufundishaji wa vijana wa Skauti ili wawe waadilifu, wawajibikaji na wazalendo kuanzia ngazi yake binafsi, katika familia, shuleni, jamii na Taifa ikiwa ni mkakati uliopo kati ya TAKUKURU na CHAMA CHA SKAUTI TANZANIA wa kuwashirikisha vijana wa Skauti katika mapambano dhidi ya Rushwa.

**Ndugu wanahabari,**

**HITIMISHO:**

TAKUKURU Mkoa wa Lindi inaendelea kuwashukuru wananchi, vyombo vya habari, pamoja na taasisi mbalimbali (binafsi na za serikali) katika Mkoa wa Lindi, kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa ofisi zetu ikiwepo kutoa taarifa mbalimbali za vitendo vya rushwa. Aidha, tunawaomba wananchi na wadau wote waendelee kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali hususani kupitia simu yetu ya dharura namba **113** bure, kwani mapambano dhidi ya rushwa si ya TAKUKURU peke yake bali ni ya jamii nzima kwa ujumla.

**Imetolewa na:**

Eng. Abnery J. Mganga

**Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi**

0738 150 118